



## TANGAZO KWA MWEZI WA URITHI KWA WAHISPANIA NA WIKI YA UKARIBISHO

**AMBAPO** Shule za Umma za Salem-Keizer zinatambua kuwa watu Wahispania na Latino/a/x na urithi wa utamaduni unachangia maendeleo ya kwenye taifa katika njia mbalimbali ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi; ni watu muhimu kwenye kilimo na nguvu kazi; wanahudumia kwenye jeshi, ni wa walimu, na ni sehemu ya wanafunzi na jamii; na

**AMBAPO** urithi wa Latino/a/x katika Amerika umeendelea kwa zaidi ya karne tano zilizopita; na

**AMBAPO** utamaduni asilia ulianzishwa hapa hata kabla Oregon haija tambulika kama jimbo; na

**AMBAPO** utamaduni wa Spaniard na Mexican ulianzishwa hapa kabla Oregon haija tambulika kama jimbo; na

**AMBAPO** Amerika ina utamaduni wa muda mrefu wa kuwakaribisha wahamiaji, ukaribisho huu umetoa faida kubwa kwa dunia, na bodi ya shule imethibitisha utamaduni huu; na

**AMBAPO** jumuiya ya Salem-Keizer Wahispania na Latino/a/x wana ndoto sawa, maadili, majaribio, na ushindi kama watu wengine na wanaonyesha jitihada na uamuzi wa kuendeleza karne zote; na,

**AMBAPO** asilimia 40 ya wanafunzi wetu na asilimia 14 ya wafanyakazi wetu wanajitambulisha kama Wahispania au Latino/a/x; na

**AMBAPO** bodi ya shule imejidhatiti kwa kutengeneza fursa kwa Wahispania na Latino/a/x; na

**AMBAPO** bodi ya shule inatoa msaada na fursa kwa wanafunzi wa Kihispania, Latino/a/x kwa kushirikiana na kushereherekea utamaduni wao kupitia MEChA, the Movimiento Estudiantil Chicano de Aztlán club, na kauli mbiu ni “umoja ni nguvu” na wengine Latino/a/x clubs na shughuli; na

**AMBAPO** shule zetu zinaheshimu na kutunza hazina ya utamaduni kwa wanafunzi wetu kupitia programu ya lugha mbili au zaidi na Urithi wetu wa Kihispania na Maendeleo ya Kozi za Kihispania. Hii itachangia kuwaandaa wanafunzi kuhitimu kwa kupata cheti cha Oregon Biliteracy, kwa manufaa ya kazi na pia vile vile kuheshimu na kuonyesha historia ya wanafunzi wetu wanaotoka kwenye familia zinazoongea Kispanshi. Hizi programu pia zinatoa fursa kwa familia wasiongea Kispanshi lakini wanahistoria nyingine ambayo itachangia muingiliano wa tamaduni tofauti katika jamii; na

**AMBAPO** jamii yetu inaimarishwa kwa kusaidiana na utetezi wa kutoka kwa Latino/a/x Salem-Keizer Coalition for Equality, Mano a Mano Family Center, Latinos Unidos Siempre, Pinos y Campesinos Unidos del Noroeste (PCUN), Causa, Instituto de Cultura Oregoniana (ICO), Interface Network, Casa de la Cultura Tlanese, Enlace, makundi ya kukuza uelewa wa uasili wa tamaduni za Mesoamerican of Indigenous Mesoamerican na FACES of America; na

**AMBAPO** ushirikishi wa maadili ya msingi kwa wilaya, na bodi ya shule inajukumu la kupinga mfumo wa historia ya ubaguzi wa kimfumo kwa Wahispania, Latino/a/x na watu wanaohamia Oregon, ambao unaendeleza kiwango cha ukosefu wa usawa kwa elimu, umasikini na kipato na matokeo ya afya yasiyolingana, hayo na yote yanaongeza migogoro ya kijamii na kiuchumi; na

**AMBAPO** bodi ya shule imethibitisha nafasi yake ya kuwa na mazingira salama naya kukaribisha katika wilaya za shule; na

**AMBAPO** ni muhimu kwa wakazi wa Salem na Keizer wakati huu kuwa pamoja na kushirikiana kwa kukumbatia talanta na mchango wa wakazi wote hususani jamii ya Wahispania na Latino/a/x; na

**AMBAPO** bodi ya shule imejidhatiti kuweka mazingira ya kuleta mafanikio mazuri kwa Wahispania, Latino/a/x na wanafunzi wahamiaji.

**BASI SASA**, Bodi ya Wakurugenzi ya shule za Umma za Salem-Keizer imetangaza Septemba 15 mpaka Oktoba 15 kuwa mwezi wa Urithi wa Kihispania na Septemba 13 mpaka 22 kuwa wiki ya ukaribisho na kuhamasisha wanao jumuiya wote kujumuika kusherehekea wanafunzi wahamiaji na familia wa Kihispania, Latino/a/x

Osvaldo Avila, Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi  
Shule za Umma za Salem-Keizer

9/14/21

Tarehe